



WALIMU WA SHULE ZA MSINGI wapokea zaidi ya shilingi milioni 200 kama bahshishi ya matokeo mazuri ya kujifunza

Mwezi Aprili mwaka 2017, walimu wa shule za msingi walioshiriki katika utafiti wa KiuFunza (Kiu ya Kujifunza) uliotekelezwa na Twaweza, walipokea malipo yenye thamani ya zaidi ya milioni 200. Malipo haya yalitokana na ufaulu wa wanafunzi wao katika majaribio ya kusoma Kiswahili na kufanya hesabu yaliyofanyika mwishoni mwa mwaka 2016. Mwanzoni mwa muhula wa masomo ya mwaka 2016, walimu hawa walipewa maelezo juu ya kanuni za utoaji wa malipo haya na kila mmoja akapewa uhuru wa kuchagua njia anayopendelea ya kupokea malipo yake, kwa akaunti ya benki au mtandao wa simu.



Kiasi kilicholipwa kwa walimu katika shule 135 kilikuwa shilingi 209,855,867.00 hivyo wastani wa malipo kwa mwalimu wa somo ulikuwa shilingi 266,315.00. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 42 ya wastani wa mshahara wa mwalimu ambao ni shilingi 637,790.00 kwa mwezi kwa mwaka 2016. Malipo ya kila mwalimu hutegemea na jinsi wanafunzi wake walivyofanya vizuri. Kiwango cha chini cha fedha kilicholipwa kilikuwa shilingi 8,100.00 ambapo ni walimu wachache tu ambao hawakuambulia kitu. Mwalimu aliyelipwa kiasi kikubwa kuliko wote alipata Shilingi milioni 3.6.

Kutoa motisha kwa walimu kwa matokeo mazuri ni wazo jipya la kisera ambalo linatoa fursa mahususi kwa wanafunzi, wazazi na mamlaka husika. Kwa wanafunzi, Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo huchangia ongezeko la ufaulu. Matokeo ya kujifunza siyo tu kipimo kizuri cha kwamba wanafunzi wamepata stadi husika, lakini pia ni dalili nzuri ya mafanikio ya baadaye ya wanafunzi hao. Matokeo ya awali ya KiuFunza yanaonesha kuwa motisha kwa mwalimu imeongeza ufaulu (matokeo ya utafiti mzima yatatolewa katikati ya mwaka 2017).

Kwa walimu, kulipwa baada ya matokeo mazuri ya wanafunzi wao hutoa fundisho kwamba kujifunza ndio lengo kuu la kwenda shule. Malipo hayo pia huwahamasisha walimu kujikita katika lengo hili na hutoa mrejesho juu ya juhudi zao. Vile vile, hii fursa kwa walimu kupata kipato cha ziada kwa kuwasaidia wanafunzi wao kuinua kiwango chya kusoma na kuhesabu.

Kwa ujumla, asilimia 91 ya walimu waliunga mkono wazo la malipo kwa walimu kutokana na matokeo mazuri (asilimia 68 wakiunga mkono kwa kiwango kikubwa zaidi). Walipoulizwa kuhusu utaratibu huu kuwa la kisera, asilimia 63 ya walimu waliafiki kwamba Serikali iweke mfumo rasmi wa motisha kwa walimu kutokana na matokeo mazuri wakati yatakapofanyika maboresho ya mishahara (lakini asilimia 37 walisema kiwango cha malipo hayo kiongezwe na kiwe sawa kwa wote).





Ni jambo jema kutambuliwa kwa jitihada za walimu na mafanikio ya kuwafanya wanafunzi wajifunze. Walimu nchini Tanzania wanakumbana na matatizo ya kutokutambuliwa na kukosa fursa, hivyo husababisha walimu wazuri kukimbia taaluma ya ualimu (hii hujitokeza pia kwenye nchi nyinginezo). Malipo kama haya ya kutambua utendaji bora yanaweza kuwavutia watu wengi wenye uwezo kitaaluma kujiunga na kazi ya walimu.

Kwa Mawaziri na mamlaka zinazohusika, Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo huongeza ufanisi na kuboresha matokeo ya elimu. Jitihada hii ya Malipo kwa Walimu baada ya Matokeo inaweza kuwa kiunganishi chanya kati ya matokeo ya kujifunza na uwekezaji wa fedha unaofanyika kwenye nyenzo za elimu kama vile mishahara ya walimu, vitabu na majengo ya shule. Motisha inaweza kubadilisha mitazamo ya walimu na uongozi wa shule katika kuboresha matokeo ya kujifunza. Pale ambapo motisha hutolewa bila upendeleo, walimu waliopo katika shule zilizopo vijijini hunufaika kwa namna ile ile wanavyonufaika walimu wenzao walioko katika shule nzuri mijini. Kuwapatia wanafunzi stadi za msingi ni muhimu kwa kila mtoto, popote pale anapojifunzia na hii hutambuliwa kwa njia ya kuwepo kwa mfumo wa utoaji motisha.



Malipo haya yanatokana na jitihada za pamoja kati ya Twaweza na Wilaya zilizotekeleza mpango huu na mamlaka zake, zikiungwa mkono na COSTECH na Wizara husika. Swali linaloongoza jitihada hii ya KiuFunza ni Je, kulipa walimu baada ya matokeo mzuri kutaleta ongezeko la kujifunza nchini Tanzania? Haya matokeo chanya yaliyopatikana yanaoana na matokeo katika nchi nyingine duniani. Baadhi ya mifumo ya shule imeanzisha au inatekeleza utafiti kuhusu kuwalipa walimu kwa matokeo mazuri. Serikali ya Tanzania imeonesha nia ya kuangalia uwezekano wa malipo kwa walimu kwa matokeo mazuri ili kunufaisha wanafunzi na walimu wengi wa K Tanzania.

Kwa taarifa zaidi kuhusu KiuFunza tafadhali tembelea <http://twaweza.org/go/kiufunza1>

